



# EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONESHA NIA: UTOAJI WA HUDUMA YA WALINZI WA USALAMA NA HUDUMA ZA MAPOKEZI KATIKA OFISI YA DAR ES SALAAM

REJEA NO. 0010007504

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) Ltd, linayaalika mashirika yenye uzoefu na yenye sifa kuonesha nia yao ya kutoa huduma za ulinzi na mapokezi kwenye mradi wa EACOP Ofisi ya Dar es Salaam. Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lilitofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mpaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, nchini Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

### MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

- Kutoa huduma za ulinzi wa saa 24/7 kwa majengo ya ofisi.
- Kutoa huduma za mapokezi wakati wa saa za kazi – sharti awe anazungumza Kiingereza.
- Kutoa huduma za ufuataliaji katika Chumba cha Udhibiti wa Usalama saa 24/7 - sharti awe anazungumza Kiingereza.
- Kutoa Msimamizi wa shughuli za Usalama aliye na bidii na mwaminifu.
- Kutoa huduma za taarifa za Kiusalama kwa Ukanda wa Afrika Mashariki, hasa Tanzania na Uganda.

### VIGEZO MUHIMU:

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi yakimbatanisha nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa ISO18788.
- Uthibitisho wa kuzingatia Kanuni za Kujitolea za Umoja wa Mataifa za Ulinzi na Haki za Binadamu (VPSHR).
- Uthibitisho kwamba taratibu za ajira zinaepuka kuajiri wafanyakazi wanaokiukaji haki za binadamu.
- Kuonesha uwezo wa kusimamia shughuli za usalama, kutoa mafunzo na kwamba anatekeleza sera thabiti ya Uwajibikaji kwa Jamii kwa mujibu wa kanuni za kazi za kitaifa.
- Sampuli ya vifaa vya mafunzo kwa walini, mtu wa mapokezi, mwendeshaji wa SCR, na msimamizi. \*
- Sampuli ya uchunguzi wa Tukio, utaratibu wa kuripoti na fomu za vielelezo.
- Rejea ya huduma alizowahi kufanya zinazofanana na hii.
- Uthibitisho wa uwezo wa kampuni kimtaji katika utoaji wa huduma.
- Uthibitisho wa leseni za Biashara na leseni zote za udhibiti au uidhinishaji unaohitajika ili kutoa huduma hizi.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na Cheti cha kuthibitisha kulipa kodi kwa mwaka uliopita.
- Wakati wa kuwasilisha maombi inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kanzidata ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa kutuma maombi haya.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufanuzi wa makampuni ya ndani.

Kumbuka; vifaa vya mafunzo vinapaswa kuwa sampuli tu, uwasilishaji wa mwongozo kamili wa mafunzo HAUTAKIWI. Hata hivyo, ni muhimu kujumuisha muhtasari wa mtaala (syllabus) na maelezo ya ratiba ya mafunzo/ratiba ya urejeaji mafunzo.

Kampuni zenyе nia, ambazo zina uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinapaswa kuonyesha nia yao kwa kutuma pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe usizidi 20Mb) mnamo au kabla ya saa **11:00** alasiri saa za Afrika Mashariki (EAT), **4<sup>th</sup> March 2022**. Kichwa cha habari sha Barua pepe kiwe ni **0010007504**.

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya (Makampuni) ya awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko wa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa taasisi za awali zenyе vigezo baada ya taasisi hizo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Maombi yote ya kuonesha nia ni lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kingereza